

# **MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

## **1.0. UTANGULIZI**

Naomba nichukue fursa hii kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha **2018/2019** ikiwa inajumuisha bajeti ya mapato na matumizi katika maeneo ya mishahara, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mpango na Bajeti hii inajumuisha mapitio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2016/2017**, mapitio ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2017/2018** hadi tarehe 31 Desemba, 2017 na maeneo ya kipaumbele kwa mwaka wa fedha **2018/2019**.

## **2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

Utekelezaji wa malengo katika bajeti ya mwaka wa fedha **2016/2017** yaliendelea vizuri na utekelezaji wa jumla ulifikia **56.6%**.

Katika mwaka wa fedha **2016/2017** Halmashauri ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya **Tzs. 32,478,042,332.02** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato na kiasi kilichokusanywa katika vyanzo vyote ni **Tzs. 28,628,816,724.07** sawa na **88.15%** kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

### **A: MAPATO**

<b>Maelezo</b>	<b>Makisio ya Mapato</b>	<b>Mapato Halisi</b>	<b>%</b>
Mapato ya ndani	1,634,773,000.00	1,694,508,366.32	103.65
Ruzuku (PE & OC)	20,559,645,999.60	19,526,143,005.00	94.97
Miradi ya maendeleo	10,283,623,332.42	7,408,165,352.75	72.04
<b>Jumla</b>	<b>32,478,042,332.02</b>	<b>28,628,816,724.07</b>	<b>88.15</b>

### **Mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

Halmashauri katika vyanzo vyake vya mapato ilipanga kukusanya mapato kiasi cha **Tzs. 1,634,773,000.00** na kiasi kilichokusanywa ni **Tzs. 1,694,508,366.32** sawa na **103.65%** kama ilivyo kwenye jedwali hapo juu.

Upungufu mkubwa wa ukusanyaji wa mapato ulionekana katika vyanzo vifuatavyo:-

<b>Na</b>	<b>Chanzo</b>	<b>Makisio ya Mapato</b>	<b>Mapato Halisi</b>	<b>%</b>
-----------	---------------	--------------------------	----------------------	----------

1.	Ushuru wa malazi	102,282,000.00	39,549,015.00	38.67
2.	Usajili wa magari madogo	8,521,000.00	3,422,000.00	40.16
3.	Ushuru wa Kunyonya Maji taka	27,360,000.00	6,314,159.00	23.08
5.	Kodi ya ardhi	80,989,000.00	22,533,626.37	27.82
	<b>Jumla</b>	<b>219,152,000.00</b>	<b>71,818,800.37</b>	<b>32.77</b>

Makusanyo hayo hafifu yalitokana na:-

- (i) Serikali ilifanya marekebisha ya sheria inayohusu ushuru wa nyumba za kulala wageni (hotel levy) ambapo ilielekezwa kuwa ushuru huo utozwe asilimia 10 badala ya asilimia 20 iliyokuwepo awali na hivyo kuathiri kiwango cha ushuru tarajiwa.
- (ii) SUMATRA ilichelewesha kuwasilisha makusanyo ya usajili wa pikipiki yaliyokuwa sehemu ya chanzo cha usajili wa magari madogo.
- (iii) Halmashauri kukosa gari la kunyonya maji taka.
- (iv) Serikali kuu kutorejsha asilimia 30 ya kodi ya ardhi iliyokusanywa na Halmashauri.

Hata hivyo vipo vyanzo ambavyo ukusanyaji wake ulizidi malengo baada ya Halmashauri kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato. Vyanzo ambavyo vilikuwa na ziada ni:-

Na	Chanzo	Makisio ya Mapato	Mapato Halisi	%
1	Ada ya Leseni za Vileo	11,640,000.00	12,554,169.39	107.85
2	Ada ya Leseni za Biashara	213,530,000.00	229,562,029.77	107.51
3	Mapato mengineyo	8,640,000.00	44,738,947.02	517.81
4	Ushuru wa Machinjio	46,980,000.00	50,620,020.00	107.75
5	Ada za usajili wa vyombo vya majini	15,263,000.00	22,984,000.00	150.59
6	Ushuru wa Samaki	60,000,000.00	122,080,602.00	203.47
7	Ushuru wa mbao za matangazo	116,124,000.00	157,758,577.28	135.85
8	Ushuru wa mabasi	119,718,000.00	123,149,500.00	102.87
9	Ushuru wa minara ya simu	22,000,000.00	29,309,472.00	133.22
	<b>Jumla</b>	<b>613,895,000.00</b>	<b>792,757,317.46</b>	<b>129.14</b>

Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka **2016/2017** ilipanga kutumia fedha kiasi cha **Tzs. 32,478,042,332.02** ikiwa ni kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo. Hata hivyo hadi tarehe 30 Juni kwa mwaka wa fedha **2016/2017**, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa imetumia **Tzs. 25,966,405,610.28** sawa na **79.95%** kama jedwali lifuatalo linavyoonesha.

## B: MATUMIZI

Maelezo	Makisio ya Mapato	Matumizi Halisi	%
Matumizi ya kawaida	21,853,219,500.74	20,476,148,117.92	93.70

(mishahara na matumizi mengineyo)			
Miradi ya maendeleo	10,624,822,831.28	5,490,257,492.36	51.67
<b>Jumla</b>	<b>32,478,042,332.02</b>	<b>25,966,405,610.28</b>	<b>79.95</b>

Katika Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha **2016/2017** Halmashauri ilikuwa na malengo **163** yaliyopangwa kutekelezwa na idara na vitengo vyake, hata hivyo Halmashauri ilifanikiwa kutekeleza malengo **99** sawa na **60.74%**. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na:-

### *Utawala*

- i. Kuendesha vikao vya kamati za kudumu za Halmashauri na kulipa stahili za waheshimiwa madiwani za kila mwezi.
- ii. Kusimamia vikao vya kisheria ngazi ya kata (WDC) na mitaa.
- iii. Kusimamia utendaji wa watumishi.
- iv. Kuandaa makisio ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka 2017/2018.
- v. Kuandaa ikama na kuiwasilisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.
- vi. Kutoa mafunzo kwa watumishi mbalimbali.
- vii. Kuendesha mashauri ya nidhamu **15** kwa watumishi wake.
- viii. Kuratibu zoezi la uhakiki wa watumishi na usajili wa vitambulisho vya Taifa kwa watumishi wa Umma.
- ix. Kuratibu zoezi la Uhakiki wa vyeti vya watumishi lililoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
- x. Kufanya uhakiki wa watumishi wa umma kwa kutumia taarifa za kitambulisho cha taifa (NIDA) pamoja na taarifa za watumishi katika mfumo wa HCMIS.

Shughuli zote zilizoainishwa hapo juu ziligharimu shilingi **700,944,774.95**.

### *Fedha na Biashara*

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na kuweza kufikia asilimia 103.65 ya makisio (makisio ya mapato yalikuwa Tzs. **1,634,773,000.00** na mapato halisi yalikuwa **Tzs. 1,694,508,366.32**)
- ii. Kuandaa taarifa za mapato na matumizi kila mwezi na kila robo mwaka.
- iii. Kuandaa na kuratibu malipo kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za fedha za Serikali za Mitaa.

- iv. Kusimamia ufungaji wa hesabu za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo zilipelekea Halmashauri kupata **Hati safi** kwa hesabu za mwaka wa fedha 2015/2016.
- v. Kujibu hoja za ukaguzi za mwaka wa fedha 2015/2016 kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.
- vi. Kutoa leseni za biashara kwa wafanyabiashara **3,011**
- vii. Kutoa leseni za vileo kwa wafanyabiashara **321**.
- viii. Kusimamia masoko **6** ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambayo hutumiwa na wafanyabiashara wadogo wadogo kutoa huduma mbalimbali za biashara za nafaka, mbogamboga, matunda, samaki, nyama na bidhaa za madukani.
- ix. Kufuatilia uzalishaji katika viwanda vikubwa.
- x. Idara kwa kushirikiana na Taasisi, Makampuni na Mashirika mbalimbali walitoa mafunzo mbalimbali yanayowalenga wafanyabiashara mbalimbali **463**.
- xi. Elimu kwa wamiliki na waendesha Pikipiki za biashara (Bodaboda) ilitolewa. Shughuli zote ziligharimu shilingi **48,868,597.65**.

### ***Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji***

Idara ilitekeleza shughuli zifuatazo;

- i. Kuratibu na kuandaa Mpango na bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2017/2018.
- ii. Kuandaa mpango kazi (Action plan) wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2016/2017
- iii. Kushiriki katika kuandaa wasifu wa Mkoa wa Mara na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- iv. Kuandaa taarifa mbalimbali kama vile za miradi ya maendeleo kila robo mwaka kwa mwaka wa fedha 2016/2017, taarifa za utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015.
- v. Kuratibu majibu ya utekelezaji wa maagizo ya viongozi mbalimbali.
- vi. Kuanza maandalizi ya Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- vii. Kutoa mafunzo juu ya Utaratibu ulioboreshwa wa Uendeshaji wa Ruzuku ya Maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGDG) kwa wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Kata (WDC).
- viii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Shughuli zote ziligharimu shilingi **78,038,500.00**.

### ***Mipango miji na Ardhi***

Shughuli zilizotekelezwa na idara ni kama ifuatavyo:-

- i. Kukamilisha kuandaa Mpango Kabambe (Musoma Master Plan 2015-2035).
- ii. Kuandaa michoro ya mipango miji 16.
- iii. Kuandaa Hati miliki 461.
- iv. Kukusanya Pango la kodi ya Ardhi na Ada zingine zitokanazo na Ardhi kiasi cha Tzs. 654,771,108.34.
- v. Kutatua migogoro ya ardhi ambapo malalamiko 162 yalipitiwa.
- vi. Kusimamia zoezi la uthamini wa mali za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- vii. Kuandaa hati za madai 2,053 ya kodi ya ardhi kwa lengo la kukusanya kodi.
- vii. Kuhamasisha na kupanda jumla ya miche **49,646** katika maeneo yafuatayo Barabara ya Majita kuanzia kituo cha polisi na Old custom, taasisi za serikali na maeneo ya watu, binafsi.
- viii. Kuhamasisha Shule za sekondari za Kiara, Nyasho na Musoma ufundi kupanda miche ya miti ya mbao na matunda.
- ix. Kufanya doria 55 kwenye mlima Mukendo ili kudhibiti ukataji wa miti.
- x. Kutunza miche ya miti katika bustani ya miche ya Mukendo (EPC).

Shughuli zote ziligharimu shilingi **106,213,463.90**.

### ***Kitengo cha Teknolojia, Habari, Mawasiliano na Uhusiano***

Shughuli zilizotekelezwa na Kitengo cha Teknolojia, Mawasiliano, Habari na Uhusiano ni:-

- i. Kuratibu na kusimamia waandishi wa Habari katika matukio kumi na sita (16) ya Halmashauri kama Baraza la Madiwani(Full Council), Utiaji saina mkataba wa ujenzi wa barabara za mjini na matukio mengine yanayohitaji kuhabarishwa kwa umma kupitia vyombo vya Habari.
- ii. Uchukuaji na uhifadhi wa matukio muhimu yaliyofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ikiwa ni picha za mnato, video na sauti.
- iii. Kitengo kilikamilisha utengenezaji wa tovuti ya Halmashauri.
- iv. Kuandika makala, kuhariri picha za mnato na video, kukusanya taarifa muhimu za idara mbalimbali kwa ajili ya kuziingiza kwenye tovuti ya Halmashauri.
- v. Kuratibu malalamiko ya wananchi ambapo malalamiko **41** yalipokelewa na kupelekwa idara husika kwa ajili ya utatuzi.
- vi. Utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA katika idara mbalimbali ili kuhakikisha usalama na utendaji kazi wake unakuwa katika hali nzuri.

- vii. Kuhakikisha mifumo ya TASAF, EPICOR, HCMIS, BEMIS na LGRCIS inakuwa katika usalama pamoja na kuendelea kufanya kazi ipasavyo. Shughuli zote ziligharimu shilingi **8,345,000.00**.

### ***Mifugo na Uvuvi***

Shughuli zilizopangwa na kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 ni:-

- i. Kuanza ukarabati wa machinjio kuu ya Bweri ambapo utekelezaji uko kwenye hatua ya awali.
- ii. Ununuzi wa chanjo za kichaa cha mbwa vichupa **100** (dozi 1,000) ambapo utekelezaji upo katika hatua ya manunuzi.
- iii. Kuimarisha ukaguzi wa afya za mifugo na mazao yake na ukusanyaji wa ushuru wa machinjio ambapo jumla ya mifugo **14,641** ilikaguliwa na nyama kuruhusiwa kwa matumizi ya binadamu.
- iv. Kufanya utambuzi wa magonjwa ya mifugo,ufuatiliaji na utoaji wa kinga na tiba kwa mifugo **16,674**.
- v. Kuingiza taarifa za mifugo na uvuvi kwenye mfumo wa ARDS za kila mwezi taarifa **12**, robo taarifa **4** na taarifa ya mwaka.
- vi. Kusimamia na kufuatilia uboreshaji wa zao la ngozi kwa kufanya ukaguzi wa mabanda 4 ya ngozi, utoaji wa vibali vya kusafirisha ngozi na bidhaa zake.
- vii. Elimu ya ufugaji bora ilitolewa kwa wafugaji **1,154** .
- viii. Kufanya doria **21** ndani na nje ya Ziwa Victoria pamoja na kutoa elimu juu ya uvuvi endelevu kwa wadau **191** walioko kwenye mialo.
- ix. Kutoa leseni za mitumbwi **287** na kukusanya mapato yatokanayo na vyanzo vya Uvuvi.
- x. Kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa samaki kwa wadau **47**.

Shughuli zote ziligharimu jumla ya shilingi **18,225,000.00**.

### ***Usafishaji na Mazingira***

Shughuli zifuatazo zilitekelezwa na idara ya Usafishaji na Mazingira;

- i. Kutoa huduma ya usafi wa mazingira kwa kufagia barabara zipatazo **297**, masoko **6** na stendi **3**.
- ii. Kusafisha na kuzibua mifereji ya maji ya mvua ipatayo **198**.
- iii. Kukusanya, kusomba na kutupa taka ngumu kutoka kwenye Kaya na vizimba zenye uzito wa tani **20,866**.
- iv. Kufyeka nyasi maeneo ya wazi mita za mraba **52** kando kando ya barabara na sehemu za wazi kudhibiti mbu, wadudu na wanyama hatari.

- v. Kufanya ukaguzi wa majengo mbalimbali **17,148** zikiwemo nyumba za kuishi, majengo ya biashara, Taasisi binafsi na za Umma na kutoa elimu ya Afya kuzingatia usafi wa mazingira.
  - vi. Kutoa huduma ya mazishi kwa marehemu **29** wasiokuwa na ndugu.
  - vii. Kufanya kaguzi katika Mitaa **73** kutambua kuwepo kwa mazalio ya mbu **680** na kuchukua hatua.
  - viii. Kukagua na kusimamia usajili wa majengo **462** kuthibiti ubora wa chakula, dawa na vipodozi.
  - ix. Kufuatilia mwenendo wa magonjwa na kutuma taarifa **48** za kuwepo au kutokuwepo kwa magonjwa hatari **12** ya milipuko.
  - x. Kuagiza na kusambaza chupa za chanjo **32,700** katika Zahanati na vituo vya Afya.
  - xi. Kuhimiza kaya **758** kuchimba, kujenga na kutumia vyoo bora na vibuyu chirizi.
  - xii. Kutoa mafunzo ya Elimu ya Afya katika mitaa **73** juu ya utupaji wa taka ngumu, taka maji na utumiaji wa vyoo bora ngazi ya kaya.
  - xiii. Kukusanya takwimu kutoka kaya **3,208** kutathimini matumizi ya vyoo bora.
  - xiv. Kuratibu zoezi la usafi wa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.
  - xv. Kufanya usimamizi elekezi kusimamia utendaji wa watumishi katika kata.
- Aidha shughuli zilizotekelezwa sehemu ya Mazingira ni kama ifuatavyo:-
- i. Kuzijengea uwezo Kamati za Mazingira za mitaa, kata na ngazi ya Manispaa.
  - ii. Kusimamia kufanyika kwa maadhimisho ya siku ya mazingira Afrika tarehe **3 Machi, 2017** na Siku ya mazingira Duniani tarehe **1-5 Juni, 2017**.
  - iii. Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa utunzaji mazingira katika viwanda vikubwa **3**, viwanda vidogo **5**, mradi wa kukoboa mpunga wa Mudeko, vituo **10** vya kuuza mafuta (petrol stations), gareji **7**, vituo **12** vya kuoshea magari (car wash), shule **5** za msingi na sekondari na vituo **3** vya kuchenjua dhahabu.
  - iv. Kutoa elimu kwa wafanyabiashara wauza samaki **13** katika mwalo wa Mwigobero kuhusu usafi wa Mazingira katika biashara zao za kuuza samaki.
  - v. Kusimamia mchakato wa tathmini ya athari kwa mazingira (**EIA na EA**) kuhusu miradi ya barabara za mjini na soko la Nyasho.
  - vi. Kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa mazingira na shughuli maalumu za kisekta zinazohusiana na mazingira.
  - vii. Kushiriki katika utungaji wa sheria ndogo za usimamizi wa mazingira za mwaka 2016.

Shughuli zote za idara ziligharimu shilingi **91,120,000.00**.

## *Afya*

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kufanya ukaguzi wa maduka ya dawa muhimu **101** na maabara **26** za watu binafsi.
- ii. Kufanya ukaguzi wa matumizi ya dawa (drug audit) katika vituo vya kutolea huduma za afya.
- iii. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya **2** na zahanati **8** ambapo dawa na vifaa tiba viliweza kununuliwa kutoka Bohari kuu ya dawa MSD.
- iv. Kufanya matengenezo ya vifaa tiba vilivyo haribika katika vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
- v. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
- vi. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
- vii. Kufanya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya wagonjwa katika vituo vya afya **2** na zahanati **8**.
- viii. Kutengeneza mabakala (shelves) ya kutunzia dawa katika stoo ya dawa ya kituo cha afya Nyasho na hivyo utunzaji wa dawa na mafaili ya wagonjwa umeboreshwa.
- ix. Kununua mafuta maalumu kwa ajili ya walemavu wa ngozi (albino) ili kuwakinga na magonjwa ya ngozi ambapo chupa za mafuta **116** zilinunuliwa na wagonjwa wa ngozi (albino) **33** waliweza kupatiwa mafuta hayo na yaliyobaki yalipelekwa katika shule ya msingi Mwisenge “B”.
- x. Kununua vifaa vya ofisi kwa ajili ya kuwapiga picha wazee na kuwatengeneza vitambulisho vya matibabu ambapo vifaa vimenunuliwa na wazee **1,702** walioko katika kata **9** wamepigwa picha na wazee **212** wamepatiwa vitambulisho vya matibabu na zoezi linaendelea.
  
- xi. Kuwawezesha watoa huduma **73** ngazi ya jamii kusajili mama wajawazito **458** na watoto **4,828** chini ya miaka mitano katika jamii.
- xii. Kufanya vikao vya kujadili vifo vya wajawazito na watoto wachanga ili kujua sababu za vifo hivyo na kuweka mikakati ya kudhibiti vifo hivyo.
- xiii. Kuchapisha kadi za kliniki (RCH) **3,000** kwa ajili ya matumizi ya vituo vya afya na zahanati katika kufuatilia ukuaji wa watoto.

- xiv. Kukusanya chupa za damu salama **625** ambapo wagonjwa **168** wenye uhitaji wa damu walipatiwa damu salama katika kituo cha afya Nyasho na hivyo kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.
- xv. Kufanya mafunzo ya siku tano kwa watumishi **22** wa afya kuhusu uchunguzi wa kansa ya shingo ya kizazi kwa wanawake.
- xvi. Kujaza Mitungi ya gesi **84** kwa ajili ya utunzaji wa chanjo katika vituo vya afya na zahanati.
- xvii. Kuwawezesha watumishi wa afya kufanya kampeni ya utoaji matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka mitano mara mbili kwa mwaka ambapo jumla ya watoto **46,032** chini ya miaka mitano walipewa huduma hiyo.
- xviii. Kununua matairi na kufanya matengenezo ya magari ya idara ya afya kwa ajili ya kuwezesha rufaa za wagonjwa na shughuli za usimimazi na chanjo ambapo magari **3** (ambulance 2 na gari la chanjo) yalinunuliwa matairi na magari Na. DFPA 2909, SM 4088, SM 4666, DFP 4385 na STK 7106 yalifanyiwa ukaguzi na kutengenezwa ili kuimarisha rufaa za wagonjwa na shughuli zingine za afya.
- xix. Kununua mafuta kwa ajili ya magari ya idara ya afya na jenereta ili kuwezesha rufaa za wagonjwa, shughuli za usimimazi, chanjo na huduma za upasuaji.
- xx. Kupima maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa wateja **1,051** (wanaume 303 na wanawake 748) katika siku ya maadhimisho ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 kati ya hao watu **9** (1%) walikutwa na maambukizo.
- xxi. Kuwawezesha watumishi wa afya 4 wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kupata lishe ili kuboresha afya zao na kuwakinga na magonjwa nyemelezi.
- xxii. Kununua vyandarua **33** vyenye viutilifu kwa ajili ya kuwapatia wagonjwa.
- xxiii. Kununua mashine ya kufulia nguo za wagonjwa katika kituo cha Afya Bweri.
- xxiv. Kujenga sehemu za kufulia nguo za wagonjwa (washing slabs) kwa ajili ya vituo vya Afya Nyasho na Bweri.
- xxv. Kusimika matenki ya maji matatu (3) katika zahanati za Buhare, Nyakato na Nyamatare kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji.
- xxvi. Kununua samani (makabati, benchi, viti na meza) za ofisi kwa ajili ya zahanati ya Nyamatare.
- xxvii. Kufanya kikao cha siku mbili cha watumishi wa afya, ustawi wa jamii na maafisa wa polisi jinsi ya kuwahudumia waanga wa ukatili wa kijinsia.
- xxviii. Kutoa zawadi ya wafanyakazi hodari 3 wa idara ya afya siku ya Mei Mosi kwa mwaka 2017.
- xxix. Kulipa stahiki mbalimbali za watumishi za watumishi wa afya **184** ambapo jumla ya watumishi **108** waliweza kulipwa stahiki zao kama likizo, fedha za

matibabu, masaa ya ziada, fedha za mazishi, sare za kazi na fedha za kusafisha mizigo kwa wastaafu.

- xxx. Kuwalipia ada watumishi **2** wanaosoma katika vyuo.
  - xxxii. Kuwezesha ofisi ya Mganga Mkuu wa manispaa kufanya kazi ambapo shajara, malipo ya bili za maji, umeme na gharama nyingine za ofisi ziliweza kushughulikiwa.
  - xxxiii. Kuitisha vikao **2** vya bodi ya afya.
  - xxxiiii. Kuitisha kikao na watumishi cha ufuatiliaji na tathmini ya utoaji huduma katika vituo **27** vya kutolea huduma za Afya.
  - xxxv. Kuwawezesha wajumbe 18 wa CHMT kufanya usimamizi elekezi/shirikishi safari 50 kwa mwaka katika vituo vya kutolea huduma za afya **27**.
  - xxxvi. Kufanya uhamasishaji katika kamati za maendeleo za kata za Iringo, Mukendo, Kitaji na Mwigobero juu ya matumizi ya madini joto na lishe ili kupunguza magonjwa yatokanayo na lishe duni.
  - xxxvii. Kuandaa mpango kabambe wa Halmashauri wa Afya (CCHP) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na Mipango **10** ya vituo vya afya **2** na zahanati **8** na kuiwasilisha OR-TAMISEMI kwa uhakiki.
  - xxxviii. Kufanya uhamasishaji wa jamii kujiunga na Mfuko wa afya wa Jamii (CHF) katika kamati za maendeleo za kata 7 (Makoko, Kamunyonge, Mshikamano, Bweri, Nyasho, Kigera na Kwangwa) na kaya **1,099 (14%)** zimejiunga katika Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) kwa mwaka 2016/2017.
  - xxxix. Kuwafanyia uchunguzi wa magonjwa ya Kichocho na Minyoo ya tumbo wanafunzi **288** wa shule 2 za msingi za Musoma na Nyasho “A” na kati ya hao wanafunzi **17** walikutwa na Minyoo ya tumbo, wanafunzi **3** walikutwa na Kichocho na wanafunzi **42** walikutwa na matatizo mengine mbalimbali na wote walitibiwa.
  - xl. Kukamilisha ujenzi ya wodi ya wazazi katika kituo cha afya Bweri na kazi inaendelea.
  - xli. Kukarabati vyumba kwa ajili ya huduma rafiki za afya kwa vijana katika vituo vya afya vya Nyasho, Bweri na Bethsaida na zahanati ya Kwangwa.
- Jumla ya fedha kiasi cha shilingi **378,625,489.00** zilitumika.

### *Elimu msingi*

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kukamilisha maandalizi ya mtihani wa Taifa wa darasa la IV, VII 2016.
- ii. Kusajili watahiniwa **4,191** wa mtihani wa Taifa Darasa VII na upimaji wa Darasa IV – 2017.

- iii. Kuratibu na kusimamia mtihani wa Taifa wa darasa VII – 2016.
  - Waliosajiliwa ni **4,191** (Wav 1,986 na Was 2,205)
  - Waliofanya mtihani ni **4,169** (Wav 1,973 na Was 2,196)
  - Waliofaulu ni **3,445** (Wav 1,765 na Was 1,680)
  - Asilimia ya ufaulu ni **82.63**.
- iv. Kuratibu na kusimamia mtihani wa darasa IV 2016.
- v. Kuandaa orodha kuu ya wanafunzi wa Kidato cha I – 2017.
- vi. Kuratibu, kusimamia na kusahihisha mtihani wa majaribio wa Mkoa Darasa VII – 2017.
- vii. Kufanya vikao, mikutano ya kiutendaji kwa Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu.
- viii. Kufanya ufuatiliaji wa utendaji kazi kwa Walimu na wanafunzi kwa Shule 52.
- ix. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa wafanyakazi bora na zawadi zao.
  - x. Kutoa mafunzo kwa walimu **54** juu ya ufundishaji wa KKK (3 Rs Inset).
  - xi. Kutoa mafunzo ya kuboresha shule (Inset General) kwa Walimu, MEK na Maafisa Elimu.
  - xii. Kutoa mafunzo ya kuziongezea Shule **38** kipato (School Income Generating activities).
  - xiii. Kuwapatia mafunzo Walimu na Waratibu Elimu Kata juu ya uongozi na utawala (School leadership and Management).
  - xiv. Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za “Capitation” na kutoa taarifa kila zinapowekwa katika akaunti za shule.
  - xv. Kuendesha semina za ukusanyaji, uandaaji na utengenezaji wa takwimu za elimu shuleni na katani kwa MEK na walimu wakuu.
  - xvi. Kutembelea Shule **42** kukagua na kuhimiza ulinzi na utunzaji bora wa mali zote za shule (Miundombinu, Samani, Vitabu, n.k).
  - xvii. Kufuatilia upatikanaji wa chakula, maji, umeme na afya za wanafunzi wenye mahitaji maalum.
  - xviii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo ya elimu ya Msingi (MEM) wa kila robo mwaka.
  - xix. Kusimamia ujenzi wa choo cha walimu na wanafunzi shule ya Msingi Mwisenge "A" chenye matundu **10** na na JWTZ Bukanga chenye matundu **10**.
  - xx. Kusimamia ujenzi na ukamilishaji wa vyumba **13** vya madarasa na choo shule ya msingi za Mwisenge “B” (04), Kambarage “A” (02), Kigera “A” (02), Rwamlimi “B” (02), JWTZ Bukanga (02) na Kapt. Msangi (02).

- xxi. Kusimamia ukarabati wa ofisi ya walimu na Ofisi ya Mwalimu Mkuu shule ya msingi Mwisenge “B”
- xxii. Kuanza ujenzi wa vyumba vya madarasa **14** katika shule za msingi za Bweri (02), Bukoba (02), Kambarage “A” (03), Kambarage “B” (02), Nyamatare “A” (01), Nyamatare “B” (01) na Mtakuja “B” (03). Hatua ya ujenzi iko hatua za msingi.

Jumla ya fedha kiasi cha shilingi **696,121,702.00** zilitumika kutekeleza kazi hizo.

### ***Elimu Sekondari***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kusimamia uwajibikaji na utendaji kazi kwa walimu na watumishi wasio walimu na kufanya tathmini ya utendaji kazi kila mwezi.
- ii. Kushiriki kuhakiki madai ya walimu kuanzia Januari, 2015 hadi Desemba, 2015.
- iii. Kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa 8 (2 Nyamiongo sekondari, 2 Iringo Sekondari na 4 Nyasho Sekondari) yamejengwa, ukarabati wa vyumba vya madarasa madarasa **14** (Nyamiongo 6, Iringo 2 na Nyasho 6), ujenzi wa matundu ya vyoo **56** (Nyasho Sekondari 10, Nyamiongo 18, Iringo 18 na Morembe Sekondari 10).
- iv. Kuendelea na ukarabati mkubwa wa majengo katika shule ya Sekondari Musoma.
- v. Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule za Sekondari (Capitation grant, Fidia ya Ada na Chakula cha wanafunzi).
- vi. Kusimamia uendeshaji wa mitihani ya Kitaifa kwa kidato cha II, IV na VI na ufaulu ulikuwa kama ifuatavyo;
  - Kidato cha II, 2016 - **94%**
  - Kidato cha IV, 2016 – **65%**
  - Kidato cha VI, 2016 – **98.2%**
- vii. Kusimamia shughuli za michezo katika shule za Sekondari ambapo wanafunzi walishiriki michezo ya UMISSETA kuanzia ngazi ya Shule, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.
- viii. Kupokea na kusambaza vifaa vya kundishia na kujifunzia (vitabu kwa shule **18** na vifaa vya maabara kwa shule **5**) katika shule za Sekondari za Serikali. Jumla ya vitabu **13,530** vya masomo ya sayansi, Hisabati Lugha na Sanaa vilipokelewa na kusambazwa katika shule za Sekondari za Serikali na vifaa vya maabara vilipokelewa kwa ajili ya shule za sekondari za Kamunyonge, Mara, Morembe, Musoma na Nyamitwebiri.
- ix. Kupanga walimu **14** wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Jumla ya fedha kiasi cha shilingi **2,431,623,999.00** zilitumika.

### ***Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kutoa mafunzo kwa wakulima **25** kuhusu kilimo bora cha zao la nyanya.
  - ii. Kuratibu hali ya chakula na upatikanaji wake.
  - iii. Kutoa huduma za ugani katika kata **16** za Manispaa ya Musoma kwa wataalamu wa ugani ngazi ya kata, kuwatembelea na kuwashauri wakulima ambapo wakulima **4,288** wa mazao ya mbalimbali katika Kata 16 za Manispaa ya Musoma walitembelewa na kupewa ushauri kuhusu kulima kwa kuzingatia kanuni bora za mazao wanayolima.
  - iv. Kukusanya takwimu za kilimo za kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka kutoka Kata **16** za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na kuziingiza katika mfumo wa Kompyuta wa "Agricultural Routine data System" (ARDS) - "Web Portal".
  - v. Kuhimiza na kuhamasisha maendeleo ya vyama vya ushirika 20 vilivyo hai ambapo jumla ya SACCOS **11** zilipata ushauri wa kisheria kupitia kikao cha pamoja kilichofanyika chini ya Mkuu wa Wilaya ambazo ni Musoma Municipal, Musoma Hospital, Musoma dairy, AIC Nyasho, Mara VETA, Mafanikio Mwigobero, Imara, Musoma Urban, Musoma, SHAMMAH na Umoja wa kahawa.
  - vi. Kuinua kiwango cha uelewa wa jamii ya vijana na vikundi vinginevyo kuhusu faida za asili za vyama vya ushirika katika kata 16 ambapo ushauri na elimu vilitolewa kwa viongozi wa vikundi 5 (Faraja-Bweri, Bora Tanzania-Mwisenge, Byangwe exploration and mining-Mkendo, Inuka-Nyakato na Maandazi-Nyasho).
  - vii. Kushiriki maonesho ya kilimo Nane nane 2016 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilipata ushindi wa nafasi ya 3 kati ya Halmashauri 36 zilizoshiriki.
  - viii. Kuandaa taarifa za mwezi, robo mwaka na kuziwasilisha kwa wadau.
- Shughuli zote ziligharimu shilingi **14,938,090,00**.

### ***Maendeleo ya jamii***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuhamasisha uundaji wa vikundi vya uzalishaji mali kutoka katika kata 16 ambapo vikundi 146 vya uzalishaji mali viliundwa.
- ii. Kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya wanawake na vijana iliyotolewa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Juni, 2017. Jumla ya Tzs. 15,739,400.00 zilirejeshwa kutoka vikundi vya wanawakenna Tzs. 3,470,000.00 kutoka vikundi vya vijana.

- iii. Kutoa mafunzo elekezi kwa vikundi vya wanawake na vijana vilivyopatiwa mikopo ambapo vikundi **75** vilipatiwa mafunzo elekezi baada kupatiwa mikopo; **54** vya wanawake na **21** vya vijana.
  - iv. Kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ambapo kaya **1,099** zilijiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii.
  - v. Kutambua asasi zisizokuwa za kiserikali ambapo asasi **4** zisizokuwa za kiserikali zilitambuliwa.
  - vi. Kufanya maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani na Siku ya Mtoto wa Afrika.
  - vii. Kusajili vikundi vya ujasiriamali **146** katika kata **16**.
  - viii. Kushughulikia kesi za ulinzi na usalama wa mtoto ambapo jumla ya kesi **162** zilishughulikiwa na kutafutiwa ufumbuzi.
  - ix. Kushughulikia mashauri **79** ya migogoro ya ndoa.
  - x. Kufanya utambuzi wa watoto wa mitaani, ambapo jumla ya watoto **18** walitambuliwa.
  - xi. Kufanya utambuzi wa watu wenye ulemavu ambapo jumla ya watu **261** wenye ulemavu wa akili, ngozi, viungo, viziwi na wasioona walitambuliwa katika kata zote **16**.
  - xii. Kufanya zoezi la upigaji picha kwa wazee kwa ajili ya kuwatengenezea vitambulisho vya matibabu, ambapo ni jumla ya wazee **1,702** walifikiwa, na **212** walipewa vitambulisho.
  - xiii. Kuendesha zoezi la uundaji wa kamati za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi (MVCC) katika kata mbili (2) za Nyakato na Mwisenge.
  - xiv. Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya na umuhimu wa upimaji wa VVU.
  - xv. Kufanya vikao na wadau na wanaoishi na VVU/UKIMWI ambapo kikao kimoja cha WAVIU na kimoja cha wadau.
  - xvi. Kutoa huduma ya upimaji wa VVU kwa hiari katika jamii ambapo upimaji wa VVU kwa watumishi wa mradi wa maji Bukanga ulifanyika.
  - xvii. Kutoa ruzuku kwa kaya maskini **2,408** zilizopo kwenye mpango.
  - xviii. Kufanya usimamizi na ufuatiliaji ngazi ya Halmashauri, Mitaa na Kata wakati wa kutoa ruzuku kwa kaya maskini **2,408**.
- Shughuli zote ziligharimu shilingi **618,226,589.00**.

### ***Kitengo cha Ugavi***

Shughuli zilizotekelezwa na kitengo cha ugavi kwa mwaka 2016/2017 ni kama ifuatavyo;

- i. Kuratibu na kusimamia ununuzi katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- ii. Kuitisha vikao vya PMU na Bodi ya Zabuni.
- iii. Kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kuzingatia sheria ya ununuzi Na. 7 ya mwaka 2011.

Shughuli zote zilizotekelezwa ziligharimu shilingi **12,924,500.00**.

## ***Maji***

Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo;

- i. Ukarabati wa miundombinu ya maji safi kwa ajili ya kuongeza wingi wa maji katika Soko kuu la Manispaa ya Musoma
- ii. Kurudisha huduma ya maji katika shule ya msingi Kapteni Msangi na soko la Nyasho.
- iii. Kufanya ukarabati wa mfumo wa maji safi na maji taka katika machinjio ya Bweri
- iv. Uwekaji wa vigae sehemu ya kuuzia samaki wabichi katika Soko Kuu.
- v. Kuweka sahani za vyoo katika shule ya sekondari Iringo na Nyamiongo
- vi. Kufanya ukarabati wa mfumo wa tanki la uvunaji wa maji ya mvua katika shule za msingi za Bukoba, Kambarage, Songambebe na Rwamlimi na shule za sekondari za Kamunyonge, Nyabisare na Morembe.
- vii. Kukarabati mfumo wa maji safi na maji taka katika nyumba 2 za Halmashauri.
- viii. Kufanya ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji katika shule za sekondari za Songe na Musoma ufundi.

Shughuli zote zilizotekelezwa kwa kutumia shilingi **15,838,625.00**.

## ***Ujenzi***

Idara ya ujenzi ilisimamia matengenezo ya barabara na ujenzi wa majengo.

## ***Kitengo cha Nyuki***

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na;

- i. Kusimamia uundaji wa kikundi kipya cha community alive.
- ii. Kuhamasisha vikundi 4 kuongeza idadi ya mizinga na kukarabati mizinga mibovu (mizinga **14** imekarabatiwa na kufanyiwa usafi).
- iii. Kuteketeza na kuhamisha makundi ya nyuki yaliyo vamaia makazi ya watu maeneo ya Free pack, Kariakoo, Airpot na Kituo cha afya cha Anglican Bweri.

Shughuli zote zilizotekelezwa ziligharimu shilingi **6,425,000.00**.

## ***Kitengo cha Sheria na Usalama***

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na;

- i. Kuendelea kusimamia kesi za madai **40** ambazo ziko katika mahakama mbalimbali (Mahakama Kuu ya Tanzania – Mwanza, Mahakama ya Wilaya –

Musoma, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya – Musoma, Mahakama ya Hakim Mkazi – Musoma na Tume ya Usuluhishi na uamuzi wa Migogoro ya kazi (CMA)).

- ii. Kupitia (vetting) mikataba mbalimbali ya Halmashauri.
- iii. Kuendelea kutoa ushauri kwa lengo la kumaliza kesi kwa kuzingatia misingi ya haki na ushauri huo ulilenga kuzuia hasara zaidi zinazoweza kujitokeza upande wa Halmashauri.
- iv. Kuondoa wafanyabiashara katika maeneo yasiyoruhusiwa maeneo ya Manota kata ya Mwigobero, Stendi ya zamani, Serengeti na Bustani ya Malkia.
- v. Kukamata mifugo iliyokuwa inazurura mjini na kutozwa faini ikiwa ni pamoja na kutoa onyo kwa wamiliki wa mifugo hiyo. Ng'ombe **180**, mbuzi **80** na kondoo **7** walikamatwa.
- vi. Kuandaa marekebisho ya sheria ndogo za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Shughuli zote ziligharimu shilingi **26,129,971.25**.

### ***Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani***

Kitengo cha ukaguzi wa ndani kina jukumu la kufanya ukaguzi wa kawaida kwa mujibu wa sheria Na. 34 ya kanuni za fedha toleo la 2001 ikisomwa pamoja na kanuni Na. 14 ya sheria za fedha ya serikali za mitaa ya mwaka 2010 (LAFM).

Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na;

- i. Kufanya ukaguzi kwa ajili ya kufanya tathimini kwa shughuli zilizofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 kwa kufanya ukaguzi wa nyaraka (Transaction Audit) na ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Lengo likiwa ni kulinganisha ufanisi wa Halmashauri na malengo ya serikali kwa madhumuni ya kuongeza umakini katika maeneo yasiyofanya vizuri, uwajibikaji na kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inafikiwa katika matumizi ya rasilimali za serikali.
- ii. Kufuatilia ili kujiridhisha kama mfumo wa udhibiti wa ndani unafanya kazi na kufuatilia hoja za nyuma.
- iii. Kuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani kwa kila robo mwaka.

Shughuli zote ziligharimu shilingi **7,714,000.00**.

Katika utekelezaji wa miradi, utekelezaji haukufanyika kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa fedha za ruzuku ya maendeleo au kutotolewa kabisa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hata hivyo utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

### ***Mapato ya Ndani (OS)***

Shughuli zilizotekelezwa ni:-

- i. Utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule za msingi na sekondari kwa Tzs. 70,168,950.00.
- ii. Kuandaa wasifu wa mkoa na Halmashauri Tzs. 19,909,000.00.
- iii. Kulipa deni la mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa Tzs. 120,000,000.00.
- iv. Kuchangia Mfuko wa maendeleo ya wanawake Tzs. 42,808,000.00 na vijana Tzs. 16,922,000.00.

### ***Mfuko wa barabara.***

Matengenezo ya barabara yalifanyika kwa kutumia fedha zilizovuka mwaka wa fedha 2015/2016 na zile zilizoidhinishwa kwa mwaka 2016/2017. Matengenezo ya barabara yaliyotekelezwa kwa kutumia fedha zilizovuka mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama yafuatayo;

- i. Matengenezo ya barabara za Magamaga, Anarlando, Nyakato, Nyabisarye, Nyakato Sa Nane, Nyakato Jumba la Dhahabu, Nyakato, Bweri maduka Tisa, Songambebe.
- ii. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Nyamatare & Kamunyonge Biafra, matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Nyamatare (Mzee Mtongori – SDA Church - Kamunyonge) na Matengenezo ya muda maalumu barabara za Haile Selasie, Peace Palace – Field Force, Kwangwa, Mara Sekondari – Kiara Buhare, Zahanati ya Kamunyonge SDA & Nyamatare, Makoko, Buhare – Mwisenge - Makoko and Buhare – Kurumuli, Makongoro na barabara za lami.
- iii. Matengenezo ya muda maalumu barabara za Buhare, Mtakuja - Nyamiongo and Mwisenge - Mjita pamoja na kalvati na mitaro barabara za Buhare, Mwisenge na Mwisenge Makaburini.
- iv. Ujenzi wa kalvati katika barabara za Kwangwa - Kiara na Kiara – Buhare na ujenzi wa mitaro na Kalvati katika barabara za Haile Selasie, Old Custom, Kawawa, Peace Palace - Field force Kwangwa na Kisurura.
- v. Ujenzi wa barabara ya lami nyepesi - FFU - Cabin - Mutex Buhare km 0.33.

Kazi zote za matengenezo ya barabara, ujenzi wa kalvati, daraja na barabara yaliyoainishwa hapo juu yalitumia jumla ya shilingi **1,297,543,306.35**.

Aidha idara ya ujenzi ilisimamia matengenezo ya barabara yaliyoanza kufanyika kwa kutumia fedha za mwaka 2016/2017. Matengenezo hayo ni kama ifuatavyo:-

- i. Matengenezo ya kawaida katika barabara za Bweri Madukatisa, Songambebe, Buhare, Nyamatare shule ya msingi - Kigera, Mtakuja – Nyamiongo, Mwisenge - Majita (Nyamrasa), Makoko, Maktaba, Nyasho, Nyakato - Mshikamano shule ya Msingi, St Anthony Makoko, Mwisenge Makaburini, Nyabisare, Mukendo, Maktaba, Kamunyonge, Kawawa, Haile Sellasie, Kitaji Bondeni, Iringo, Nyasho Majita, Nyamatare, Mukendo SDA Church, Kusaga, Majengo Mapya na Bweri Paroma,
- ii. Matengenezo ya sehemu korofi katika barabara za Kamunyonge, Bethsaida na Kigera, Buhare, Mwisenge - Misango, Mtakuja – Makaburini, Makoko ziwani, Iringo, Old Custom, Kitaji, Nyasho, Magamaga, Nyakato sanane na Rwamlimi,
  - i. Matengenezo ya Muda maalumu katika barabara za Kwangwa, Kamunyonge, Kiara – Buhare, Nyamatare, Sokoni (Shomoro), Kusaga, Mukendo, Shabani, Uhuru, Sokoni, Boma, Nyasho Cabin, Welfare, Mshikamano, Nyakato Sanane, Songambebe, Bweri - Nyamitwebiri, Majengo – Rwamlimi, Songe - Kambarage – Iringo sekondari, Kwangwa na Mara Sekondari - Kiara,
  - ii. Ujenzi wa mitaro katika barabara za Kiara – Buhare, Kwangwa, Bethsaida, Mwisenge - Misango, Mtakuja – Makaburini, Makoko ziwani, Old Custom, Welfare, Nyasho Cabin, Majita - Makaburini, Mwisenge Makaburini, Bukanga, CCM - NMB (Polisi), Mwigobero, Mwisenge Misango, Iringo, Nyasho Cabin - Magereza, Nyasho - Magereza, Nyasho Majita & Nyamatare, Kwangwa - Kiara, Bweri Maduka Tisa, Buhare Bima na Kiara Gengeni.
- iii. Ujenzi wa daraja barabara ya Mshikamano- Rwamlimi.

Kazi zote ziligharimu **Tzs. 1,602,200,950.96.**

### ***Programu ya Uboreshaji wa Miji (ULGSP)***

Shughuli zilizotekelezwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Miji ni:-

- i. Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Nyasho – Majita km 2.38.
- ii. Kupitia upya usanifu barabara zenye urefu wa km 10.15 ili kuendana na fedha tarajiwa kupokelewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.
- iii. Kutafuta mhandisi mshauri wa kusimamia ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 10.15.
- iv. Kupitia na kuhuisha mkataba wa huduma kwa mteja Tzs. 18,231,000.00.
- v. Kununua kompyuta mpakato 8, mashine kubwa ya kurudufu moja, “projector” na “screen board” yake Tzs. 18,231,000.00.
- vi. Mafunzo kuhusu ushirikishwaji na mgawanyo wa madaraka kwa kuzingatia jinsia na utawala bora kwa waheshimiwa madiwani na wakuu wa idara Tzs. 4,142,500.00.

- vii. Mafunzo ya kamati za maendeleo za kata 16 kuhusu wajibu wa serikali za mitaa katika uhifadhi na usimamamizi wa mazingira Tzs. 7,574,000.00.
- viii. Kutoa mafunzo kwa wenyeviti na watendaji wa mitaa na watumishi kuhusu usimamamizi wa fedha na ushirikishwaji wa jamii katika ngazi za mitaa Tzs. 15,049,000.00.
- ix. Kuanza uboreshaji wa barabara zenye urefu wa km 9.867 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Tzs. 9,930,059,618.54 na Mkandarasi ni M/S Nyanza Road Works. Aidha kazi ya kusimamia uboreshaji wa km 9.867 utafanywa na Mhandisi mshauri ambaye ni Norplan Co. Ltd kwa gharama ya shilingi 873,000,000.00.

### ***Ruzuku ya Maendeleo (LGDG)***

Shughuli zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za ruzuku ya maendeleo ni:-

- i. Kuanza ukamilishaji wa wodi ya wazazi kituo cha afya Bweri Tzs. 22,695,275.00.
- ii. Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi Kigera "A" (2), Rwamlimi "B" (2), Kapteini Msangi (2) na JWTZ Bukanga (1) Tzs. 103,549,000.00.
- iii. Kuandaa na kusambaza taarifa kwa wadau zikiwemo za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) n.k. Tzs. 5,815,000.
- iv. Ufuatiliaji na usimamamizi kwa miradi inayotekelezwa Tzs. 15,040,000.00
- v. Kuandaa na kuwasilisha Mpango na Bajeti katika mamlaka husika Tzs. 19,780,000.00.

### ***Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF)***

Shughuli iliyotekelezwa ni:-

- i. Kununua mabati 1,332 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za msingi Tzs. 30,399,000.00.

### ***Programu ya kudhibiti UKIMWI***

Shughuli zilizotekelezwa ni:-

- i. Kuelimisha jamii jinsi ya kujikinga na maambukizi ya VVU, umuhimu wa upimaji wa VVU na matumizi sahihi ya ARVs kwa njia ya sinema. Tzs. 4,792,500.00.
- ii. Kumwezesha CHAC kuhudhuria vikao vya mkoa na kanda Tzs. 1,120,000.00.
- iii. Kuendesha ofisi ya CHAC kwa kunua vitendea kazi Tzs. 995,000.00.
- iv. Kuimarisha na kusaidia kamati za kudhibiti UKIMWI ngazi ya kata na mtaa katika kuratibu shughuli za kudhibiti UKIMWI Tzs. 9,825,000.00.

- v. Kufanya vikao vya wadau na mtandao wa wanaoishi na VVU/UKIMWI Tzs. 1,950,000.00.
- vi. Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya shughuli za kudhibiti UKIMWI Tzs. 4,960,000.00.
- vii. Kuwezesha CMAC kufanya ufuatiliaji wa shughuli za kudhibiti UKIMWI Tzs. 3,990,000.00.
- viii. Kukusanya, kuunganisha na kutuma taarifa za “TOMSHA” za robo ya nne Tzs. 750,000.00.

***Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEDP)***

- i. Uboreshaji wa miundombinu ya shule za sekondari za Iringo na Nyamiongo umekamilika. Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha **Tzs. 162,408,196.00** za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari na zilitumika.

***Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF)***

Shughuli kwa kutumia fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya ni zifuatazo:-

- i. Ununuzi wa Madawa na Vifaa tiba kwa vituo vya afya viwili (2) na zahanati nane (8).
  - ii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji (physical and financial progress implementation reports) za robo mbili kwa mwaka wa fedha 2016/2017 katika mamlaka husika.
  - iii. Kufanya maandalizi ya awali ya kuandaa Mpango Kamambe wa Afya (CCHP) kwa mwaka wa fedha 2017/2018.
  - iv. Kuwezesha watumishi katika vituo vya Afya kutoa huduma kwa masaa 24.
  - v. Kuwezesha watumishi 4 wanaoishi na VVU kupata lishe.
  - vi. Kufanya matengenezo ya magari 3 ya idara ya afya.
  - vii. Kufanya usimamizi elekezi katika vituo 27 vya kutolea huduma za afya.
  - viii. Kufanya matengenezo ya vifaa tiba katika vituo vya afya 2 na zahanati 1.
  - ix. Kuwawezesha watumishi waliotoa huduma za mkoba kwa mitaa iliyo mbali na vituo vya kutolea huduma za afya.
  - x. Kuwezesha rufaa kwa wagonjwa kutoka zahanati kwenda vituo vya afya na kutoka vituo vya afya kwenda Hospitali ya Mkoa.
  - xi. Kuwezesha mtumishi mmoja kuongeza ujuzi katika taaluma zao.
  - xii. Kuanza usimikaji wa matenki kwa ajili ya kutunzia maji katika zahanati tatu (3) za Nyakato, Nyamatara na Buhare.
- Shughuli zote zimegharimu **Tzs. 79,489,887.00**.

### ***Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC)***

#### **Shughuli iliyotekelezwa ni:-**

- i. Kukamilisha ujenzi wa kliniki za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU na wajawazito na watoto. Kliniki zote zimeanza kutoa huduma kwa wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Fedha zilizotumika ni **Tzs. 947,750,000.00.**

### **Mpango wa Elimu kwa Matokeo (EPforR)**

#### Shughuli zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

- i. Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa, choo cha matundu 10 na Ofisi 2 za walimu shule ya msingi Mwisenge "B" Tzs. 101,000,000.00.
- ii. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya msingi Kamarage "A" Tzs. 13,000,000.00.
- iii. Ujenzi wa chumba 1 cha darasa na choo chenye matundu 10 shule ya msingi JWTZ Bukanga Tzs. 28,792,714.00.
- iv. Ukarabati wa jengo la utawala, ujenzi wa matundu ya vyoo 10 na vyumba 4 vya madarasa katika shule ya sekondari Nyasho, ujenzi wa matundu ya vyoo 10 shule ya sekondari Morembe na ukamilishaji wa ujenzi wa maabara 2 shule ya sekondari Makoko Tzs. 122,705,809.00.

### ***Programu ya Equip – Tanzania***

#### Shughuli zilizopangwa kwa mwaka 2016/2017 ambazo zilitekelezwa ni:-

- i. Kuendesha mafunzo ya KKK Tzs. 50,436,765.000.
- ii. Kuwezesha ushirikiano kati ya Jamii na Shule Tzs. 48,297,674.00.
- iii. INSET gharama ya Mikataba ya walimu wawezeshaji Tzs. 3,600,000.00.
- iv. INSET General/shughuli za kawaida Tzs. 41,793,000.
- v. Kutoa ruzuku ya shughuli za uzalishaji shuleni Tzs. 19,590,000.00.
- vi. Uongozi na utawala shuleni Tzs. 24,809,570.00.
- vii. Ruzuku ya Waratibu Elimu Kata Tzs. 34,644,930.

### ***Mpango wa TASAF III***

#### Kupitia Mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia TASAF III shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

- i. Kutoa elimu kwa walengwa 2,408 juu ya matumizi ya fedha ambayo hupewa hususani kwa kuzielekeza kwenye biashara ndogondogo, kilimo na ufugaji ili kuweza kujiinua kiuchumi na kukabiliana na changamoto za maisha katika kaya zao.

- ii. Kupokea na kugawa ruzuku ya kiasi cha **Tzs. 612,006,584.99** inayotolewa kwa kaya maskini 2,408. Jumla ya fedha kiasi cha **Tzs.14,704,000.00** zilirudishwa kwenye akaunti ya TASAF kutokana na baadhi ya walengwa kutofika kuchukua fedha zao kwenye kituo cha malipo na wengine kuondolewa kwenye mpango kwa sababu za vifo na kukosa vigezo vya kuwa kwenye mpango.
- iii. Kuingiza kwenye mfumo fomu za madai na marekebisho.
- iv. Kutembelea kaya na kuona shughuli wanazozifanya za kujiongezea kipato.
- v. Kukusanya fomu za masharti ya elimu na afya na kuziingiza katika mfumo.

Katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha **2016/2017** Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo pia utatuzi wake umeainishwa:-

<b>Na</b>	<b>Changamoto</b>	<b>Utatuzi</b>
1.	Kuchelewa/Kutotolewa kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na fedha za uendeshaji wa Halmashauri (OC).	Serikali kuu iombwe kutoa fedha kwa mujibu wa mpango kazi wa Halmashauri
2.	Upungufu wa watumishi hususan katika idara za Afya, Elimu msingi na sekondari na Mipango miji	Kufuatilia vibali vya ajira na kuajiri watumishi
3.	Upungufu wa vitendea kazi	Kununua vitendea kazi
4.	Uhaba wa magari ya kusomba taka ngumu na maji taka	Ununuzi wa magari
5.	Mabadiliko ya tabia nchi yaliyoathiri uzalishaji wa mazao ya chakula na malisho ya mifugo	Kuimarisha hifadhi ya mazingira, kulima mazao yanayostahimili ukame na kupanda malisho ya mifugo

### **3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya **Tzs. 38,437,660,060.41** kwa ajili ya kuyatumia kutekeleza mpango na bajeti yake na hadi tarehe 31 Desemba, 2017 kiasi kilichokuwa kimekusanywa katika vyanzo vyote ni **Tzs. 15,157,174,858.30** sawa na **39.43%** kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

## A: MAPATO

Maelezo	Makisio ya Mapato	Mapato Halisi	%
Mapato ya ndani	1,953,273,000.00	852,817,142.04	43.66
Ruzuku (PE & OC)	23,190,249,859.58	8,799,958,917.25	37.95
Miradi ya maendeleo	13,294,137,200.83	5,504,398,799.01	41.40
<b>Jumla</b>	<b>38,437,660,060.41</b>	<b>15,157,174,858.30</b>	<b>39.43</b>

### Mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2017/2018 katika vyanzo vyake vya mapato ilipanga kukusanya mapato kiasi cha **Tzs. 1,953,273,000.00** lakini kiasi ilichokusanya hadi tarehe 31, Desemba 2017 ni **Tzs. 852,817,142.04** sawa na **43.66%**. Vyanzo ambavyo vinaonekana kuwa na upungufu wa mapato hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

Na	Chanzo	Makisio	Mapato	%
1	Ushuru wa Huduma	299,101,000.00	140,746,170.07	47.06
2	Ushuru wa Malazi	69,062,000.00	26,327,261.00	38.12
3	Ada za Maombi ya zabuni	16,300,000.00	2,160,070.00	13.25
4	Ushuru wa uoshaji magari	6,120,000.00	2,495,000.00	40.77
5	Ushuru wa machinjio	47,980,000.00	23,431,300.00	48.84
6	Ushuru wa Mitumbwi	25,000,000.00	5,738,000.00	22.95
7	Ushuru wa samaki	145,800,000.00	38,774,241.00	26.59
8	Ada ya usafi	130,542,000.00	2,807,480.00	2.15
9	Gharama ya uchangiaji huduma za Afya	144,036,000.00	41,840,080.00	29.05
10	Ushuru wa madini ya ujenzi	60,000,000.00	4,358,500.00	7.26
11	Ushuru wa mbao za Matangazo	116,124,000.00	1,187,866.66	1.02
12	Kodi ya ardhi	80,989,000.00	50,000.00	0.06
	<b>Jumla</b>	<b>1,141,054,000.00</b>	<b>289,915,968.73</b>	<b>25.41</b>

Upungufu huo wa mapato uanatokana na sababu zifuatazo:-

- i. Serikali kutorejesha asilimia 30 ya kodi ya ardhi inayokusanywa.
- ii. Ushuru wa mbao za matangazo kuondolewa katika vyanzo vinavyo kusanywa na Halmashauri na sasa unakusanywa na TRA.
- iii. Mwitikio mdogo wa wananchi kulipia ada ya usafi na kujiunga na mfuko wa afya ya jamii.
- iv. Kukosekana kwa gari la Halmashauri la kunyonya maji taka.
- v. Mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha upungufu wa samaki.
- vi. Kazi za matengenezo ya barabara kusimamiwa na TARURA imeathiri mapato yatokanayo na ada za maombi ya zabuni.

Hata hivyo vipo vyanzo ambavyo hadi tarehe 31 Desemba, 2017 ukusanyaji wake uliendelea vizuri. Vyanzo hivyo ni kama ifuatavyo:-

Na	Chanzo	Makisio	Mapato	%
1	Ushuru wa Masoko	14,342,000.00	7,836,878.00	54.64
2	Kodi ya vizimba	288,383,000.00	180,766,910.00	62.68
3	Ada za leseni za vileo	13,240,000.00	6,951,064.00	52.50
4	Ada ya usajili wa magari	8,521,000.00	10,874,000.00	127.61
5	Ushuru wa maegesho	28,776,000.00	17,510,000.00	60.85
6	Ada za leseni za Biashara	219,130,000.00	181,324,440.37	82.75
7	Ada za shule	90,790,000.00	52,465,000.00	57.79
8	Ushuru wa stendi ya mabasi	119,718,000.00	61,782,000.00	51.61
9	Ushuru wa minara ya simu	29,319,000.00	15,722,064.00	53.62
	<b>Jumla</b>	<b>812,219,000.00</b>	<b>535,232,356.37</b>	<b>65.90</b>

Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilipanga kutumia fedha kiasi cha **Tzs. 38,437,660,060.41** ikiwa ni kwa ajili ya kulipa mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo hadi tarehe 31 Desemba, 2017 Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ilikuwa imetumia **Tzs. 12,486,511,513.95** ikiwa ni sawa na **32.49%** ya fedha zilizokisiwa kama jedwali linavyoonyesha hapa chini:-

#### **B: MATUMIZI**

MAELEZO	MAKISIO	MATUMIZI	%
Matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo)	24,122,414,575.58	9,355,711,221.80	38.78
Miradi ya maendeleo	14,315,245,484.83	3,130,800,292.15	21.87
<b>Jumla</b>	<b>38,437,660,060.41</b>	<b>12,486,511,513.95</b>	<b>32.49</b>

Katika Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilikuwa na malengo **157** yaliyopangwa kutekelezwa na idara na vitengo, hata hivyo Halmashauri hadi tarehe 31 Desemba, 2017 imefanikiwa kutekeleza sehemu ya malengo **65**. Miongoni mwa shughuli ambazo zimetokelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na:-

#### **Utawala**

- i. Kusimamia utendaji wa watumishi 1,647.
- ii. Kuendesha vikao vya Kamati za kudumu na Baraza la Manispaa na kulipa stahili za waheshimiwa madiwani za kila mwezi.
- iii. Kufuatilia na kuratibu vikao vya kata 16 na mikutano ya mitaa 73.

- iv. Kuratibu na kusimamia ziara ya mafunzo ya Kamati ya Fedha na Uongozi iliyofoyanyika katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Manispaa ya Shinyanga.

### ***Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji***

Shughuli zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

- i. Kuratibu na kuandaa Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
- ii. Kufanya maandalizi ya tathmini ya mwaka ya miradi ya LGDG.
- iii. Kushiriki katika kuandaa Wasifu wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- iv. Kuandaa taarifa mbalimbali kama vile za miradi ya maendeleo robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2017/2018, taarifa za utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015-2020.
- v. Kuratibu majibu ya utekelezaji wa maagizo ya viongozi mbalimbali.
- vi. Kuandaa Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- vii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- viii. Kuratibu na kuendesha mafunzo ya PlanRep mpya na FFARS kwa watendaji wa Halmashauri ya Manispaa.

Shughuli zote zimegharimu **Tzs. 9,592,000.00**.

### ***Fedha na Biashara***

Shughuli zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

- i. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambapo kufikia tarehe 31 Desemba, 2017 Halmashauri ilikuwa imekusanya asilimia 43.66 ya makisio ya mapato yake.
- ii. Kuandaa taarifa za mapato na matumizi kila mwezi na kila robo mwaka.
- iii. Kuandaa na kuratibu malipo kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za fedha za Serikali za Mitaa.
- iv. Kusimamia ufungaji wa hesabu za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.
- v. Kujibu hoja za ukaguzi za mwaka wa fedha 2016/2017 kwa wakati na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.
- vi. Kutoa leseni za biashara kwa wafanyabiashara **1,988**.
- vii. Kutoa leseni za vileo kwa wafanyabiashara **141**.

- viii. Kusimamia ushuru wa huduma (service levy), ushuru wa malazi, masoko na kukusanya mapato yatokanayo na kodi ya vibanda.
  - ix. Kufuatilia mwenendo wa bei ya bidhaa katika masoko yetu ya Manispaa.
  - x. Kufuatilia uzalishaji wa bidhaa katika viwanda vikubwa.
- Shughuli zote ziligharimu **Tzs. 53,381,061.00.**

### ***Kitengo cha Teknolojia, Habari, Mawasiliano na Uhusiano***

Shughuli zilizotekelezwa na kitengo ni:-

- i. Kuratibu na kusimamia waandishi wa Habari katika matukio kumi na sita (16).
- ii. Uchukuaji na uhifadhi wa matukio muhimu yaliyofanyika katika Halmashauri ikiwa ni uchukuaji wa picha za mnato, video na sauti. Jumla ya picha za mnato 217, video 31 pamoja na uchukuaji wa sauti (audio recording) ‘Clips’ 16 umefanyika.
- iii. Kuendelea kusimamia tovuti ya Halmashauri. Uingizaji na uhuishaji wa taarifa katika tovuti hufanyika mara kwa mara. Jumla ya taarifa 43 ziliingizwa katika tovuti.
- iv. Kuandika makala, kuhariri picha za mnato na video, kukusanya taarifa muhimu za idara mbalimbali kwa ajili ya kuziingiza kwenye tovuti ya Halmashauri umefanyika ambapo makala 9, Habari 14 zimeandikwa na kuwekwa katika tovuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- v. Kuratibu malalamiko ya wananchi ambapo malalamiko 67 yalipokelewa na kupelekwa idara husika kwa ajili ya utatuzi na malalamiko 49 yamekamiliwa na 18 yako katika hatua mbalimbali za utatuzi.
- vi. Kutengeneza vifaa vya TEHAMA katika idara mbalimbali ili kuhakikisha usalama na utendaji kazi wake unakuwa katika hali nzuri.
- vii. Kitengo kimehakikisha mifumo ya TASAF, EPICOR, HCMIS, BEMIS na LGRCIS inakuwa katika usalama pamoja na kuendelea kufanya kazi ipasavyo.

Shughuli zote zimegharimu **Tzs. 5,330,000.00.**

### ***Afya***

Shughuli zilizotekelezwa na idara ni:-

- i. Kutayarisha taarifa ya utekelezaji ya robo ya kwanza na pili (Julai- Septemba na Oktoba- Desemba 2017) za Mpango Kabambe wa Halmashauri wa Afya (CCHP) 2017/2018 na kuiwasilisha wizara ya Afya na OR-TAMISEMI.
- ii. Kutoa huduma za Afya kwa wagonjwa **61,641** waliofika katika vituo vya kutolea huduma za afya kupata matibabu kama wagonjwa wa nje. Kati ya hao

wagonjwa **6561** walilazwa na wagonjwa **796** walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa matibabu zaidi.

- iii. Kuwahudumia mama wajawazito **2,290** waliofika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kujifungua, kati yao mama wajawazito **19** walifanyiwa upasuaji katika kituo cha afya Nyasho.
- iv. Kutoa huduma ya chanjo kwa watoto walio chini ya miaka mitano ambapo watoto **3,700** walipatiwa huduma hiyo ambayo ni sawa na **152%** ya walengwa **2,430** kwa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).
- v. Kugawa vyandarua kwa mama wajawazito **3,037** wa hudhuria la kwanza na watoto chini ya miaka mitano **3,714** waliohudhuria kliniki ili kuwakinga na mbu waenezo Malaria.
- vi. Kutoa dawa za matone ya Vitamini A kwa akina mama **950** na watoto **15,211** waliofika vituoni kupata huduma hiyo katika kipindi cha miezi 6.
- vii. Kufanya maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani, ambapo upimaji wa VVU ulifanyika kwa wateja **783** na waliokutwa na maambukizi walikuwa **10** sawa na asilimia **1.3%**.
- viii. Kufanya usimamizi elekezi katika vituo **27** vya kutolea huduma za Afya vilivyondani ya Halmashauri ya Manispaa na changamoto zilizoibuliwa zimepatiwa ufumbuzi.
- ix. Kufanya uhamasishaji wa jamii kuchangia damu na kiasi cha chupa **167** zimeweza kukusanywa na wagonjwa 99 wenye uhitaji wa damu salama wameweza kuongezewa damu katika kituo cha afya Nyasho.
- x. Kuwapiga picha wazee **4,983** kati ya wazee **7,100** waliotambuliwa katika kata **16** kwa ajili ya kuwapatia vitambulisho vya matibabu na wazee **3,378** wameshapatiwa vitambulisho vyao vya matibabu na zoezi linaendelea ili kuwafikia wazee wote ambao hawakupata nafasi ya kupigwa picha.
- xi. Kufanya uhamasishaji wa jamii kujiunga na mfuko wa Afya ya jamii (CHF) ambapo kaya **496** zimejiunga na mfuko wa afya ya jamii katika vituo vya afya **2** na zahanati **8**, na hivyo kufikisha kaya **4,124** zilizojiunga na CHF kati ya kaya **27,059 (15%)**.
- xii. Kufanya ukaguzi wa maduka ya dawa, ambapo jumla ya maduka **94** yalikaguliwa na maduka **37** yalikutwa na makosa mbalimbali na hivyo yalifungwa.
- xiii. Kukamilisha ujenzi wa jengo la kujifungulia na kuanza kutumika katika kituo cha afya Bweri.

Kazi zote hizi zimegharimu kiasi cha **169,247,955.00**.

## *Usafishaji na Mazingira*

Idara ya Usafishaji na Mazingira imeendelea kufuatilia na kusimamia huduma za Afya ya Mazingira ili kupambana na magonjwa ya kuambukiza na ya milipuko katika jamii. Kwa kipindi zha Julai hadi Desemba 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa;-

- i. Kuzibua mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa km.108.
- ii. Kukusanya, kusomba na kutupa taka ngumu zenye uzito wa tani 14,196.
- iii. Kutoa huduma ya Usafi wa Mazingira kwa kufagia barabara zenye urefu wa km 151.
- iv. Kufanya ukaguzi wa majengo mbalimbali 9,628 zikiwemo nyumba za kuishi, majengo ya biashara, makampuni na taasisi.
- v. Kufanya ukaguzi katika mitaa 73 ili kutambua kuwepo kwa mazalio ya mbu na kuchukua hatua za kuzuia malaria.
- vi. Kufanya kampeni ya kitaifa ya Usafi wa Mazingira kuhusu ujenzi na matumizi ya vyoo bora katika Kata 16 zilizo chini ya mpango.
- vii. Kutoa huduma ya mazishi kwa marehemu 21 wasiokuwa na jamaa
- viii. Kutoa mafunzo ya elimu ya Afya katika mitaa 73 juu ya utupaji wa taka ngumu na taka maji, uchimbaji na ujenzi wa vyoo bora,uwepo wa vibuyu chirizi na kuvitumia.
- ix. Kukagua na kusajili majengo 95 yanayotumika kuandaa na kusambaza vyakula.
- x. Kukusanya sampuli za maji 24 na 12 za vyakula na kuzipeleka kwa mkemia Mkuu wa Serikali kuhakiki ubora wake.
- xi. Kufuatilia na kutuma takwimu za kuwepo magonjwa hatari ya mlipuko
- xii. Kufyeka nyasi mita za mraba 108.
- xiii. Kufanya usimamizi elekezi katika kata 16 ambapo masuala mbalimbali ya kiutendaji yalipatiwa ufumbuzi.
- xiv. Semina elekezi ilitolewa kwa Watendaji wa Mitaa 73 na Wenyeviti wa Mitaa 73 ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kuhusu wajibu wao katika usimamizi wa mazingira.
- xv. Udhibiti wa uchimbaji holela wa madini ujenzi katika eneo la mto kata ya Buhare ulifanyika.
- xvi. Ofisi ya mazingira ilitoa maoni kwa maandishi kuhusu mpango wa kusimamia masuala ya kimazingira na kijamii (site specific ESMP) kwa Mtaalamu Mshauri wa mradi wa ujenzi wa barabara za mjini (9.867km) kwa kiwango cha lami (Norplan (T) Ltd)
- xvii. Kushiriki katika kufanya mapitio (review) ya mkataba wa huduma kwa mteja (**service charter**).

xviii. Udhhibiti wa uchimbaji holela wa madini ujenzi katika eneo la bonde la mto Mgaranjabo, kata ya Buhare.

Shughuli zote ziligharimu **Tzs. 30,357,204.00.**

### *Elimu ya Msingi*

Katika kuboresha taaluma katika shule za msingi shughuli zifuatazo zimefanyika:-

- i. Kutembelea na kukagua shule za kata ya Bweri, Kigera, Nyasho, Kamunyonge na Mwisenge.
- ii. Kuhakiki na Kusaini **TSM 9** kwa wanafunzi wa darasa la saba **2017** kwa Shule **50** za Manispaa.
- iii. Kupokea, Kugawa, kusimamia na kukabidhi Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba **2017** uliofanyika tarehe **06** na **07/09/2017**.
- iv. Kusimamia ukarabati wa vyoo vya walimu, wanafunzi na karakana shule ya Msingi Mwembeni 'A'.
- v. Kukusanya Takwimu za maoteo ya uandikishaji wa wanafunzi darasa la kwanza 2018 kutoka mitaa **73** ya Manispaa ya Musoma.
- vi. Kupokea na kugawa vifaa vya wanafunzi wenye ulemavu kutoka UNICEF na TEA.
- vii. Kusimamia shughuli za uezekaji wa vyumba 16 vya madarasa katika shule za Kambarage 'A', Nyamatara 'A', Nyamatara 'B', Kigera 'A', Nyarigamba 'A', Rwamlimi 'B', Bweri na Mtakuja 'B'.
- viii. Kusimamia mafunzo ya kuhesabu moduli ya 5 – 9 yaliyofanyika shule ya msingi Mwembeni 'B'. Walimu Wakuu 38, Walimu mahiri wa kuhesabu 38, Waratibu Elimu Kata 16 na Waratibu wa mafunzo ngazi ya shule 38 walihudhuria.
- ix. Kusimamia na kuendesha mafunzo ya utayari wa kujiunga na elimu ya msingi (SRP) Mwembeni. Walimu wa darasa la kwanza 38, Waratibu Elimu Kata 16 na Walimu wa Vituo vya utayari 30 walihudhuria.
- x. Kushiriki mafunzo ya utayari kwa ajili ya kuanza Elimu ya Sekondari (SSRP) Bunda. Waratibu Elimu Kata 4 na Walimu 4 walihudhuria.
- xi. Kuendesha na kusimamia mafunzo ya wajibu na majukumu ya Waratibu Elimu Kata kwa waratibu 16.
- xii. Kutembelea na kukagua maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji katika shule za Msingi za Mwisenge 'B', Kigera 'A', Buhare, Kambarage 'A' na 'B', Kamunyonge 'A', Nyarigamba 'A' na Songambe.
- xiii. Kushiriki shughuli maalum ya kuwapangia shule wanafunzi waliofaulu kujiunga na Sekondari za Bweni na Kutwa. Wanafunzi **3,739** kati yao

- Wavulana **1,965** na Wasichana **1,774** walichaguliwa kujiunga na sekondari kati ya Wanafunzi **5,015** waliofanya mtihani sawa na asilimia **74.56** ya ufaulu.
- xiv. Kusimamia ukamilishaji wa maboma manne yatakayo kamilishwa na **EQUIP Tanzania** kwa kushirikiana na **OR TAMISEMI** kwa shule za Msingi za Kamunyonge 'A' na Kambarage 'B'.
  - xv. Kuteua maeneo yasiyo na mgogoro ili kujenga shule shikizi tatu kwa Msaada wa **EQUIP Tanzania** na **OR TAMISEMI**, Maeneo yaliyochaguliwa ni Nyabisare, Bweri na Makoko
  - xvi. Kupokea na Kusimamia Ufanyikaji wa Mtihani wa Darasa la **IV 2017** wa Taifa ambapo wanafunzi **4,542** kati yao Wavulana ni **2,151** na Wasichana ni **2,391** walifanya mtihani huo.
  - xvii. Usimamizi na Ufuatiliaji wa vituo vya **MEMKWA** pamoja na ukaguzi wa ufundishaji kwa kutumia zana.
  - xviii. Kuchagua na kuteua Walimu Wakuu **26** kwa kuzingatia viwango vya Elimu kama ilivyoagizwa katika waraka wa Elimu uliotolewa na **OR TAMISEMI**.
  - xix. Kupokea na kugawa vifaa vya wanafunzi walemavu wa Shule ya Msingi Mwisenge 'B' kwa ajili ya Darasa la **I** na **II**.
  - xx. Kuanza uandikishaji kwa wanafunzi wa darasa la Awali na la Kwanza 2018, hali halisi ya uandikishaji hadi kufikia Desemba 2017 ni asilimia **91.72** kwa Darasa la awali na kwa Darasa la kwanza ni asilimia **99.35**.
  - xxi. Kusimamia na kukagua ujenzi na ukarabati katika shule za msingi ambapo vyumba vya madarasa **16** vilipauliwa, misingi **19** na maboma **08**.
  - xxii. Kushiriki Mashindano ya watu wenye ulemavu '**Special Olympic**' yaliyofanyika Zanzibar Mwezi wa **12, 2017**.
- Shughuli hizi ziligharimu **Tzs. 371,583,444.00**.

### *Elimu ya Sekondari*

Idara ya Elimu Sekondari katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2017 imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- i. Kusimamia matumizi ya fedha za chakula kwa shule tatu **3** za bweni, fedha ya ruzuku (capitation) kwa shule **18** na fedha ya fidia.
- ii. Kufanya ufuatiliaji na kusimamia utendaji na uwajibikaji kazini kwa walimu katika shule za Sekondari.

- iii. Kusimamia mtihani wa majaribio (Mock) ngazi ya Mkoa kwa kidato cha IV, 2017.
  - iv. Kusimamia ujenzi wa uzio katika shule ya Sekondari ya wasichana Songe.
  - v. Kuandaa orodha ya walimu 106 walioomba likizo na waliostahili malipo.
  - vi. Kusimamia mitihani ya kidato cha II na IV jumla ya watahiniwa **2,975 (Me 1,636, Ke 1,339)** wa kidato cha pili na watahiniwa **2,529 (Me 1,479, Ke 1,050)** wa kidato cha IV walifanya mtihani.
  - vii. Kushiriki zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha I – 2018 ambapo jumla ya wanafunzi **2,739** waliofaulu mtihani wa darasa la VII walichaguliwa kujiunga na shule za Sekondari.
  - viii. Kushiriki kwenye mchakato wa kuandaa bajeti ya mwaka wa fedha **2018/2019**.
  - ix. Kushiriki katika mchakato wa kununua, kupokea na kukagua vifaa vya karakana katika shule ya sekondari Musoma Ufundi.
- Jumla ya fedha iliyotumika ni **Tzs. 1,050,766,562.00**.

### ***Maji***

Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kufikia Desemba, 2017 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kupeleka maji katika vyoo vya walimu na wanafunzi katika shule ya msingi Kamnyonge “A”.
- ii. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji safi na maji taka katika vyoo vilivyopo katika Ofisi kuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.
- iii. Kujenga na kuweka mfumo wa maji taka sehemu ya kutumbulia samaki wabichi na sehemu ya kuweka tanki la maji ya akiba katika Soko Kuu.
- iv. Kufanya ukarabati wa mfumo wa maji safi na maji taka katika kituo cha afya Nyasho, zahanati ya Nyamatara, Bweri na nyumba anayoishi Mkurugenzi.
- v. Kujenga matanki ya kuvunia maji ya mvua matatu (3) katika shule za Sekondari Iringo na Nyasho na Zahanati ya Rwamlimi.

Shughuli zote zilitekelezwa kwa kutumia shilingi **21,691,175.00**.

### ***Maendeleo ya Jamii***

Shughuli zilizotekelezwa na idara ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuunda vikundi vya ujasiriamali na vya kijamii. Ambapo jumla ya vikundi **70** viliundwa.
- ii. Kuhakiki vikundi **55** (wanawake **41** na vijana **14**) vilivyoomba mikopo.
- iii. Kutoa mafunzo elekezi kwa vikundi **21** vya wanawake na **8** vya vijana kabla ya kupewa mikopo.

- iv. Ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana umefanyika.
  - v. Kesi **55** za ulinzi na usalama wa watoto zimeshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi.
  - vi. Kesi za migogoro ya ndoa **32** zimeshughulikiwa na kutafutiwa ufumbuzi, kesi **7** za ulinzi na usalama wa watoto zimepatiwa rufaa kwenda Mahakama ya Mwanzo Kitaji na rufaa **1** ya mtoto mchanga ilitolewa kwenda kwenye makao ya kituo cha kulea watoto wadogo kilichopo Bweri ambaye alifiwa na mama yake mzazi mara tu baada ya kuzaliwa.
  - vii. Kuadhimisha siku **16** za kupinga ukatili wa kijinsia.
  - viii. Kuadhimisha siku ya viziwi duniani kimkoa katika Manispaa ya Musoma kwa kushirikiana na chama cha viziwi Tanzania (CHAVITA).
  - ix. Kuwezesha na kushiriki maadhimisho ya siku ya wazee duniani ambapo Wawakilishi **2** wa wazee na Afisa Ustawi wa Jamii waliwezesha kuhudhulia maadhimisho kitaifa mkoani Dodoma tarehe 1/10/2017.
  - x. Kutambua vikundi 30 vya ujasiriamali.
- Shughuli zote ziligharimu **Tzs. 4,310,000.00**.

### ***Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika***

Shughuli zilizotekelezwa na idara ni kama ifuatavyo:-

- i. Kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa maafisa ugani 12 ngazi ya kata.
- ii. Kusimamia na kutoa ushauri wa kitalaam katika vikundi vya wakulima vya UWABWE na Nyakamitu vinavyolima mazao ya mboga mboga katika vitalu nyumba.
- iii. Kutoa huduma za ugani katika kata kwa kutembelea na kufundisha kuhusu kanuni bora za kilimo wakulima 1,458.
- iv. Kufundisha wakulima 124 kuhusu njia mbalimbali za umwagiliaji.
- v. Kuingiza taarifa za kilimo katika mfumo wa “Agricultural Routine Data System – Web Portal.”
- vi. Kushiriki katika maonesho ya kilimo mseto yaliyofanyika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Maonesho hayo yaliandaliwa na VI Agroforestry na AICT.
- vii. Kutoa ushauri wa kisheria kuhusu usimamizi wa shughuli za kila siku katika vyama vya ushirika 10.
- viii. Kuhudhuria na kutoa ufafanuzi wa sheria katika vikao vya kamati na mikutano mikuu katika vyama 11
- ix. Kutoa elimu na kuhamasisha kikundi kimoja (1) kuhusu faida za asili za vyama vya ushirika na taratibu za uanzishwaji wake.

- x. Kuandikisha chama kimoja cha ushirika.
  - xi. Kutoa elimu kupitia mikutano mikuu katika vyama 5.
  - xii. Kuandaa taarifa za kila mwezi na robo ya pili ya mwaka 2017/2018.
- Shughuli zote ziligharimu **Tzs. 22,342,510.00.**

### ***Mifugo na Uvuvi***

Idara ya Mifugo na uvuvi kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- i. Kusimamia ukarabati wa machinjio ya Bweri.
- ii. Kutoa chanjo kwa mbwa 322.
- iii. Kutambua, kusajili na kupiga chapa ng'ombe 2,227.
- iv. Kufanya ukaguzi wa afya za wanyama na mazao yake ambapo mifugo 14,641 iliruhusiwa kuchinjwa na nyama kukaguliwa na kuruhusiwa kwa matumizi ya binadamu.
- v. Kufuatilia na kutambua magonjwa ya mifugo na kutoa kinga na tiba kwa mifugo 16,674.
- vi. Kutoa huduma ya elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji 1,154.
- vii. Kuingiza taarifa za mifugo na uvuvi kwenye mfumo wa ARDS.
- viii. Kufuatilia na kusimamia uboreshaji wa zao la ngozi kwa kufanya ukaguzi wa mabanda 4 ya ngozi, utoaji wa vibali vya kusafirisha ngozi na bidhaa zake.
- ix. Kufanya doria 11 ndani na nje ya ziwa Victoria pamoja na kutoa elimu juu ya uvuvi endelevu kwa wadau 205 walioko katika mialo na mabwawa ya ufugaji wa samaki.
- x. Kutoa leseni za mitumbwi 48 na ukusanyaji wa samaki.
- xi. Kutoa elimu ya ufugaji bora wa samaki kwa wafugaji wa samaki 126.

Shughuli zilizotekelezwa ziligharimu **Tzs. 14,245,750.00.**

### ***Mipango miji na Ardhi***

Shughuli zilizotekelezwa na idara ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuandaa Hati miliki za viwanja 319.
- ii. Kusimamia urasimishaji wa maeneo matatu (3) ya Songe, Nyabisarye na Buhare kati na tayari ramani zimerudishwa na upimaji unaendelea katika maeneo mawili (2).
- iii. Kutatua migogoro ya ardhi 42.
- iv. Kumilikisha viwanja 323.

- v. Kufanya ukaguzi wa maeneo 187 ili kubaini wananchi waliokiuka sheria ya kutoendeleza kwa wakati.
  - vi. Kuandaa michoro ya Mipango Miji 20.
  - vii. Kugawa miche 6,982 kwa jamii kwa ajili ya kupanda.
- Shughuli zote ziligharimu **Tzs. 4,025,000.00.**

### ***Kitengo cha Nyuki***

Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki kwenye kikundi cha Community Alive chenye wanachama 41.
- ii. Kuhamasisha ufugaji wa nyuki kata ya Bweri mtaa wa Bukoba.

Kwa upande wa miradi, utekelezaji haukufanyika kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hata hivyo utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

### ***Mapato ya Ndani (OS)***

- i. Kufanya ukaguzi, tathimini na usimamizi wa miradi ya maendeleo Tzs. 38,421,103.00
- ii. Kulipa deni la mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa Tzs. 60,000,000.00.
- iii. Kutengeneza madawati (3 seaters) kwa ajili ya shule za msingi Tzs. 13,545,000.00.
